**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI ZA MAENDELEO KWENYE HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO**

## 1.0 UTANGULIZI

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Kwa niaba ya wananchi wa Halmashauri ya Mji Makambako, nachukua fursa hii kukupongeza kwa kuteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa wa Njombe na pia tunakukaribisha sana kwenye Halmashauri ya Mji Makambako.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Halmashauri ya Mji Makambako ni moja ya Halmashauri sita zilizopo katika Mkoa wa Njombe. Halmashauri ilianzishwa rasmi tarehe 01.07.2012 na ina ukubwa wa eneo la kilomita za mraba 883.7. Sehemu kubwa ya eneo hili takribani asilimia 80 liko nje ya Mji katika kata za Mahongole, Kitandililo, Utengule na asilimia takribani 20 ndio iko katika kata za Mjini ambazo ni Makambako, Lyamkena, Kivavi, Kitisi, Mwembetogwa, Maguvani, Majengo, Mjimwema na Mlowa.

Halmashauri ya Mji Makambako inapakana na Wilaya ya Mufindi kwa upande wa Kaskazini na sehemu za upande wa Mashariki, upande wa Magharibi inapakana na Wilaya ya Wanging'ombe. Upande wa Kusini na sehemu za upande wa mashariki inapakana na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Makambako ina kadiriwa kuwa na jumla ya wakazi 116,398 kati yao Wanaume 55,522 na Wanawake 60,876 kwa ongezeko la wastani wa 3% kwa mwaka. Wakazi hawa wa Makambako wanajishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi zikiwa ni pamoja na; Kilimo, ufugaji, biashara na viwanda vidogovidogo.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Njia kuu za usafiri zinazotegemewa ni barabara kuu ya Mbeya – Dar es - Saalam na Makambako – Songea zote zinapita katika Mji wa Makambako na reli ya TAZARA inayotoka Dar es Salaam hadi Zambia.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Halmashauri ya Mji Makambako ina tarafa moja, Kata 12, Vijiji 14, Mitaa 54 ,Vitongoji 67 na jimbo moja la uchaguzi. Watumishi walioajiriwa na serikali wapo 1314 ikiwa wanaume ni 569 na wanawake ni 745. Idara zilizopo ni 13 na vitengo ni 6.

Waheshimiwa madiwani wanaowakilisha wananchi wa Makambako kwenye baraza la madiwani la Halmashauri wapo 17 ikiwa madiwani 12 ni wakuchaguliwa na madiwani 5 ni wakuteuliwa pamoja na Mheshimiwa Mbunge wa jimbo la Makambako.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Halmashauri ya Mji Makambako inaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo zinazolenga kuboresha hali ya maisha ya wananchi kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza kikamilifu shughuli zilizopo kwenye mpango na bajeti ya Halmashauri ya Mwaka 2019-2020 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020.

Taarifa hii imejikita kueleza jinsi Halmashauri inayoendelea kutekeleza Mpango na Bajeti ya Mwaka 2019/2020 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020. Hivyo, ufafanuzi wa hali ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali kisekta ni kama ifuatavyo:-

## 2.0 Sekta ya Elimu Msingi;

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Halmashauri ina shule za Msingi na awali **38** za serikali na shule 2 za binafsi zenye jumla ya wanafunzi **26,969** kati yao wavulana ni **13,205** na wasichana ni **13,764**.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Hali ya Miundo mbinu ya madawati, vyumba vya madarasa na nyumba za Walimu katika Shule za Msingi za Serikali ni kama ifuatavyo; Mahitaji ya madarasa **632** yaliyopo ni **341** na upungufu **291** na nyumba za walimu mahitaji **632**, zilizopo **180** upungufu **452.**

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Katika mtihani wa Taifa wa darasa la saba wa Mwaka 2019 Halmashauri ya Makambako ilishika nafasi ya kwanza kimkoa kwa kufaulisha wanafunzi 2489 sawa na asilimia 93.85 ya ufaulu. Aidha, ufaulu huu ni sawa na ongezeko la asilimia 2.86 toka mwaka 2018 ambapo ufaulu ulikuwa asilimia 90.99.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Idadi ya wanafunzi wa darasa la awali ambapo wameandikishwa hadi sasa ni 2318 ikiwa wavulana ni 1174 na wasichana ni 1144 sawa na asilimia 70 ya malengo. Aidha, jumla ya wanafunzi 3902 wa darasa la kwanza wameandikishwa sawa na asilimia 108.66 ya

malengo ikiwa wavulana ni 1970 na wasichana ni 1932. Uandikishaji wa darasa la awali na darasa la kwanza unaendelea hadi tarehe 31/03/2020.

### 2.1.0 Mikakati ya Kupunguza Upungufu wa Miundombinu kwenye Shule za Msingi

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

i. Jumla ya **Tshs. 38,000,000.00** zimetengwa kutoka mapato ya ndani kwa mwaka 2019-2020 kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa madarasa 18 na ofisi 8 kwenye shule za msingi 9 ambapo kiasi cha **Tsh 24,500,000** zimeshatolewa kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa madarasa na ofisi.

ii. Serikali kuu kupitia mfuko wa kunusuru kaya maskini imeweza kujenga madarasa 2,Ofisi na Vyoo vya wanafunzi na walimu katika shule ya Msingi Majengo.

iii. Kuendelea kuhamasisha Wananchi kuchangia utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya shule za Msingi ambapo mwitikio wa wananchi katika kushiriki shughuli za maendeleo unaendelea kuongezeka kwa kiasi kikubwa.

### 2.2.0 Mapato na Matumizi ya Fedha za Mpango wa Elimu bila Malipo (Elimu Bure)

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2019 Halmashauri imeshapokea jumla ya **Tshs. 87,487,456** fedha za Elimu bila Malipo kwa ajili ya elimu ya Msingi kwa mwaka 2019/2020 . Aidha, fedha zote zilizopokelewa zimetumika kwenye kugharamia uendeshaji wa

shule, posho ya madaraka za walimu wakuu na maafisa elimu Kata pamoja na kugharamia chakula cha mchana kwa wanafunzi wenye ulemavu.

## 3.0 Sekta ya Elimu Sekondari

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Katika Halmashauri kuna jumla ya shule za sekondari 16 , kati ya hizo zipo za serikali 10 na watu binafsi 6. Aidha, katika shule za Serikali, walimu waliopo ni 371 wanaume 218 wanawake 143. Aidha, kuna upungufu wa walimu 43 kwa walimu wa masomo ya sayansi, Hisabati na walimu wa masomo ya sanaa hakuna upungufu.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Hali ya Miundo mbinu ya vyumba vya madarasa na nyumba za walimu katika Shule za Sekondari za Serikali; Mahitaji ya vyumba vya madarasa ni 174 yaliyopo 156 pungufu 18 na nyumba za walimu mahitaji 361 zilizopo 36 , upungufu 325, Matundu ya vyoo vya wanafunzi mahitaji ni 306, yaliyopo ni 234, upungufu 82, Daharia mahitaji 52, yaliyopo 9, upungufu 43 na Bweni mahitaji 4, yaliyopo 3, upungufu 01.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Katika matokeo ya kidato cha nne kwa mwaka 2019 Halmashauri imeshika nafasi ya 54 kati ya Halmashauri 195 kwa kuongeza nafasi 15 kutoka nafasi ya 69 mwaka 2018. Aidha,Kimkoa Halmashauri imeshika nafasi ya 3 kati ya Halmashauri sita.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Idadi ya wanafunzi walioripoti kidato cha kwanza hadi sasa kwa mwaka 2020 ni 1891 ikiwa wavulana ni 806 na wasichana ni 1085.

Aidha, kati ya wanafunzi walioripoti, wanafunzi wenye mahitaji maalum ni 33 ikiwa wavulana ni 23 na wasichana ni 10.

### 3.1.0 Elimu bila Malipo Sekondari

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2019 Halmashauri imepokea kiasi cha **Tshs. 164,173,291.33** ikiwa ni kwa ajili ya Fidia ya Ada, Posho za madaraka za wakuu wa Shule na fedha za chakula cha wanafunzi.

### 3.2.0 Mikakati ya Kupunguza Upungufu Miundombinu ya Shule za Sekondari

i. Jumla ya **Tshs. 26,000,000.00** zimetengwa kutoka mapato ya ndani kwa ajili ya kuchangia ujenzi wa madarasa 16 na Ofisi 8. Aidha, kiasi cha **Tsh 26,000,000** kimeshatolewa kuchangia ujenzi wa madarasa kwenye shule za Sekondari.

ii. Halmashuri ilitenga kiasi cha **Tshs. 10,000,000.00** kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili kutengeneza madawati 200 na kiasi chote cha fedha kimeshatolewa na utengenezaji wa madawati unaendelea.

iii. Kuhamasisha jamii katika ngazi ya Kata na Vijiji/Mitaa kuunga jitihada za serikali kupunguza upungufu wa madarasa na Ofisi ambapo wananchi wanaendelea kuchangia ujenzi wa madarasa 17 na ofisi 8 kwenye shule mbalimbali.

## 4.0 Sekta ya Kilimo

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Uzalishaji wa chakula kwa msimu wa kilimo wa mwaka 2018/2019 ni jumla ya **tani 22,998.25** ambapo mahitaji ya chakula ni tani 22,260.46 kwa mwaka. Hivyo, Halmashauri ilikuwa na ziada ya chakula ya jumla ya **tani 737.79**.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Hali ya upatikanaji wa mbolea aina ya DAP ni nzuri. Aidha, upatikanaji wa mbolea aina ya UREA siyo nzuri. Hadi kufikia tarehe 27/01/2020 kulikuwa na tani 1082 za mbolea ya DAP na mbolea ya UREA imeisha katika maghala na maduka ya makampuni na mawakala wa pembejeo.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Halmashauri imeendelea kutekeleza agizo la bei elekezi ya mbolea kwa kutangaza bei elekezi zote za mbolea kwa wananchi na wafanyabiashara pamoja na kufanya ufuatiliaji na ukaguzi wa maduka ya pembejeo.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Vilevile Halmashauri ya Mji Makambako imeendelea kutekeleza agizo la serikali la kufuatilia madeni ya mikopo kwenye vyama vya ushirika ambapo hadi kufikia tarehe 22/01/2020 jumla ya wadaiwa sugu 38 wamekamatwa na kufikishwa mahakamani.

Aidha kufuatia zoezi hilo kiasi cha **Tsh 240,148,776.00** kimerudishwa kati ya **Tsh 764,943,901.00.**

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Katika sekta ya kilimo Halmashauri inakabiliwa na changamoto zifuatazo; Uhaba wa mbolea ya UREA yenye bei elekezi na Uwepo wa mvua nyingi ambazo zimeathiri mazao ya wakulima

## 5.0 Sekta ya Ardhi

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Halmashauri ina viwanja **8151** vilivyopimwa na kusajiliwa na Mkurugenzi wa Upimaji na ramani**.** Katika viwanja hivyo viwanja

**5712** vimeandaliwa hati miliki na hati hizo zimeshatolewa kwa wenye viwanja hivyo. Pia, Halmashauri imetoa leseni za makazi **67** kuanzia Julai 2019 hadi Disemba 2019 ili kuwasaidia wananchi kutambulika na kuthaminika kwenye taasisi zinazotoa mikopo mbalimbali. Leseni hizo zimekuwa zikitolewa kwenye maeneo yaliyojengwa kiholela. Maeneo hayo sasa yameanza kurasimishwa, hivyo tunategemea kuacha kutoa leseni hizo mara tu zoezi la kurasimisha litakapokamilika.

Vilevile, Halmashauri ya Mji Makambako inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kurasimisha makazi holela na kupanga Mji kwenye maeneo ambayo yalikuwa hayajapimwa ambapo imeweka malengo ya kurasimisha viwanja elfu kumi (10000) na mpaka sasa zoezi hili limekamilika katika mitaa sita (6). Jumla ya viwanja 1845 sawa na asilimia 18 vimeshapimwa na kuandaliwa hati miliki.

## 6.0 Sekta ya Maji

### 4.1.0 Hali ya Upatikanaji wa Huduma ya Maji ya Bomba Vijijini

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Huduma ya maji vijijini inatolewa katika kata 3 zenye jumla ya vijiji 14 ambapo mpaka sasa jumla ya vijiji 7 sawa na asilimia 50 vinapata huduma ya maji ya bomba. Huduma ya maji vijijini inatolewa kwa wakazi 17,132 kati ya 28,175 sawa na asilimia 60.8 ya wakazi wote waishio vijijini. Miradi ya maji inasimamiwa na vyombo vilivyosajiliwa Kisheria (COWSOs) na Kamati za maji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo kupitia Programu ya maji na usafi wa mazingira imewekeza kwenye miradi ya maji kwa kujenga miundombinu, ambapo kwa kipindi cha mwaka 2015 – 2018 Ujenzi wa skimu za maji vijijini na miundombinu uligharimu kiasi cha **Sh. 1,679,777,002.52** Miundombinu hiyo ni kama ifuatavyo:

(i) **Mradi wa maji ya bomba Manga**: Mradi huu unahudumia jumla ya wakazi 3,665 kwa sasa katika kijiji cha Manga na sehemu ya kijiji cha Mahongole na unakadiriwa kuhudumia watu 6,245 (population projection) miaka 20 ijayo. Mradi una vituo vya kuchotea maji kumi na sita (16), tanki moja lenye ujazo wa lita 75,000, urefu wa Mtandao ni km 41.8.

(ii) **Mradi wa uchimbaji wa visima virefu sita (6) vya maji:** Visima hivyo vimechimbwa katika vijiji vya Mtulingala, Nyamande, Ibatu, Mahongole, Ikelu na Kiumba. Ujenzi wa miradi hii inaendelea na ipo katika hatua tofauti tofauti ya ujenzi. Miradi hii itakapokamilika itahudumia jumla ya wakazi 12,051 waliopo sasa na makisio ya idadi ya watu 20,533 (population projection) miaka 20 ijayo. Miradi hii itakuwa na jumla ya vituo vya kuchotea maji Hamsini na tatu (66), Matanki matatu yenye ujazo wa lita 150,000 kila moja, tanki moja lenye ujazo wa lita 100,000, jumla ya urefu wa mtandao ni km 76.25 Wananchi 25 wameunganishiwa maji kwenye nyumba zao.

(iii) **Mradi wa Maji mtiririko Usetule/Mahongole**: Mradi huu utahudumia jumla ya wakazi 4,266 waliopo sasa, mradi huu utakuwa na vituo vya kuchotea maji ishirini na moja (28),

Matanki mawili yenye ujazo wa lita 150,000 kila moja, urefu wa mtandao km 52.2. Mradi huu utakapokamilika utahudumia jumla ya wakazi 7,269 kufikia (population projection) miaka 20 ijayo.

(iv) **Mradi wa ukarabati, matengenezo na upanuzi wa miradi ya maji vijijini:** Mradi huu unahusisha vijiji vya Manga, Mahongole Utengule na Ngamanga. Miradi hii itaboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa jumla ya wakazi 4,750.

## 7.0 Sekta ya Afya

Halmshauri ina hospitali 1 ya taasisi ya dini, vituo vya afya 2 na zahanati 11 kati ya hizo za serikali 4 taasisi za dini 4 na watu binafsi 4. Aidha, Halmashauri imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ili kuboresha huduma za Afya kwa wananchi kama ifuatavyo:-

i. Halmashauri inaendelea na ujenzi wa zahanati 13 ambapo kwa Mwaka 2019/2020 Halmashauri imetoa kiasi cha **Tsh 32,389,000** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa zahanati ya Usetule, Ibatu, Mtanga na Ngamanga na kiasi cha **Tsh 50,305,000** kimetolewa Kukamilisha ujenzi wa Jengo la wagonjwa wa nje Kituo cha Afya Lyamkena.

ii. Halmashauri ilipokea kiasi cha **Tsh 400,000,000.00** kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa majengo matano ;jengo la Maabara, jengo la Mama na Mtoto, jengo la Kufulia, Nyumba ya Mtumishi na jengo la Upasuaji. Aidha, kiasi cha **Tsh**

**399,982,767.20** kimeshatumika na ujenzi wa Majengo yote umekamilika.

iii. Halmashauri ilipokea **Tsh 1,500,000,000** kutoka serikali kuu kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Mji Makambako katika kata ya Mlowa. Aidha, Mpaka sasa kiasi cha **Tshs 1,499,024,595.28** kimeshatumika kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba na ujenzi upo asilimia 98 ya ukamilishaji. Aidha, ukamilishaji unaendelea kwa kutumia fedha za mapato ya ndani.

iv. Ujenzi wa zahanati ya Kilimahewa na zahanati ya Kitisi upo hatua ya Ukamilishaji ambapo mradi unatekelezwa na fedha za mfuko wa maendeleo ya jamii TASAF.

v. Ujenzi wa duka la dawa na chumba cha mionzi katika kituo cha Afya Makambako unaendelea.

## 8.0 Utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Kupitia TASAF kwa Mwaka wa fedha 2018/2019.

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2018/2019 Halmashauri imehaulisha fedha kwa kaya masikini kwa vipindi vitatu ambapo imelipa jumla ya **Tshs. 337,481,228.00** kwa walengwa 2282. Aidha, Kiasi cha **Tsh 1,284,578,108.88** zimepokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa Nyumba (2) za walimu, Jengo la utawala, Ujenzi wa madarasa 2 na Vyoo matundu 6, ujenzi wa zahanati 2, ujenzi wa hosteli 2, ujenzi wa barabara za Mitaa na Vijiji, ujenzi wa jengo la kufulia na ununuzi wa mashine za kufulia. Aidha,

baadhi ya miradi imekamilika na miradi mingine ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji.

## 9.0 Mfuko wa Wanawake na Vijana

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Kwa mwaka 2019/2020, hadi kufikia 31 Desemba, 2019 Halmashauri imeshatoa kiasi cha **Tsh 91,500,000**.00 kwenye vikundi **54** vya Vijana **Tsh 32,500,000**, vikundi **32** vya Wanawake **Tsh 56,000,000** na **Tsh 3,000,000** vikundi **2** vya watu wenye ulemavu kwa awamu ya kwanza. Aidha, kwa awamu ya pili Halmashauri imeshatenga kiasi cha **Tsh 130,500,000** kwa ajili ya kukopesha vikundi **97** vilivyofanyiwa uhakiki. Vilevile, Halmashauri imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Tsh 58,259,000** ikiwa ni marejesho ya mikopo kutoka kwenye vikundi mbalimbali vilivyokopeshwa fedha na Halmashauri.

## 10.0 Hali ya Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Kwa mwaka wa fedha **2019/2020** Halmashauri ya Mji Makambako ilikusudia kukusanya kiasi cha T**Sh 2,639,910,110** kutokana na vyanzo vyake vya ndani, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2019 Halmashauri imekusanya kiasi cha T**Sh. 1,438,181,457.45** sawa na **asilimia 54.48** ya lengo kwa mwaka. Aidha, Michango ya wananchi na Nguvu za Kazi kwa mwaka wa fedha ilikadiriwa kuchangia kiasi cha **Tsh 500,000,000** ambapo hadi Desemba, 2019 kiasi cha **Tsh 188,535,100** kimechangiwa sawa na asilimia **18.6.**

## 10.1 Mikakati Kuongeza Mapato ya Halmashauri

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Halmashauri ina mikakati ifuatayo ya kuongeza mapato ya ndani:-

i. Ujenzi wa Maghala 120 kwa kushirikiana na wananchi
ii. Kubuni na kusimamia vyanzo vipya vya mapato (Stendi kuu ya Mabasi katika eneo la Kipagamo, Masoko 4, Maegesho ya Malori, Mnada wa Majengo na Soko la Mbao Idofi)
iii. Wakuu wa Idara kuhusika moja kwa moja kukusanya mapato mara tatu kwa kila wiki.
iv. Kuongeza mashine za kukusanyia mapato (POS)

## 11.0 HITIMISHO

***Ndugu Katibu Tawala Mkoa***

Natoa shukrani za dhati kwa kuja kututembelea.Vilevile, ni matumaini yetu kwamba ziara yako itakuwa na mchango mkubwa hasa katika jitihada za utekelezaji shughuli za maendeleo ya wananchi wa Makambako.

Naomba kuwasilisha.

**Rashid Njozi**

Kaimu Mkurugenzi

**Halmashauri ya Mji Makambako**